HALMASHAURI YA MJI MASASI

MJI WETU-FAHARI YETU

Jarida la Mtandaoni | Toleo Maalum | www. masasitc.go.tz | Machi 2021-2025

# KISHINDO CHA MINNE YA RAIS SAMIA HALMASHAURI MJI MASASI



## TAHARIRI



**Halmashauri** ya Mji Masasi ni moja kati ya Halmashauri tisa zilizopo ndani ya Mkoa wa Mtwara na ilianzishwa rasmi mwaka 2012. Halmashauri hii ina jumla ya Kata 14, Vijiji 31, Mitaa 57 na Vitongoji 149 na kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 ina watu 137, 585 wakiwemo wanawake 71, 804 na wanaume 65,781.

Mji wa Masasi ni Kitovu cha biashara mkoani Mtwara na katika kipindi cha Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Halmashauri ya Mji Masasi imeendelea kwa kasi na ufanisi wa kiwango cha juu.

Katika kipindi cha miaka minne Halmashauri imeshuhudia mageuzi makubwa kwa kupokea fedha nyingi za miradi ya maendeleo ambayo yote tumeikamilisha na inatumika na wananchi kuanzia sekta ya elimu, afya, utawala, kilimo, mifugo, uvuvi, mpango wa kunusuru kaya masikini, mikopo ya asilimia kumi, viwanda, biashara, uwekezaji, mazingira, miundombinu, upimaji ardhi, teknolojia, na mawasilino .

***Nawakaribisha** kusoma Jarida hili ambalo linaangazia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.*

***Reuben Sixbert Jichabu***
***Mkurugenzi wa Mji Masasi***
***Julai 2025.***

©Halmashauri ya Mji Masasi, Julai 2025

HALIUZWI

# YALIYOMO


- Tahariri......................................................................................1
- Utekelezaji wa miradi kwa muhtasari.............................................3
- Mhe. Waziri ashangazwa na kasi ya utekelezaji wa miradi..................4
- Uzinduzi wa zahanati tatu kwa kishindo,wananchi wanufaika..........5
- Dc Masasi aeleza mafanikio sekta ya maji na barabara.......................7
- Ujenzi wa miundombinu ya kisasa Mkomaindo..................................8
- Wajumbe wa kamati ya bunge wapongeza kituo cha afya mtandi.......9
- Utekelezaji wa miradi ya maendeleo umefanyika kwa kasi.................11
- Rc Mtwara alikabidhi madawati 1500, Rekodi ya kihistoria.................13
- Baraza la wazee masasi lapongeza ubora wa Huduma za afya...........15
- Dondoo muhimu za utekelezaji sekta ya elimu sekondari....................16
- Dondoo muhimu za utekelezaji sekta ya elimu msingi.........................18
- Dondoo za mafanikio sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji.........19
- Dondoo za mafanikio sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.......................20
- Dondoo za mafanikio sekta ya fedha.................................................20
- Dondoo za mafanikio sekta ya usafi wa Mazingira..............................21
- Utekelezaji wa miradi ya maendeleo 2024/2025................................22
- Uwezeshaji wananchi kiuchumi.........................................................23
- Utekelezaji wa mradi wa ufungaji wa taa za barabarani........................23
- Ukarabati wa kisasa wa uwanja wa boma unaendelea.........................24
- Matukio katika picha.......................................................................25


*Tembelea Tovuti yetu kupata Nakala yako/www.masasitc.go.tz*

*"Skani kusoma"*

# UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA MUHTASARI





**KATA**

MKUTI

MKOMAINDO

NAPUPA

NYASA

MTANDI

MIGONGO

JIDA



**KATA**

SULULU

CHANIKANGUO

TEMEKE

MUMBAKA

MWENGEMTAPIKA

MATAWALE

MARIKA





- Ruzuku kutoka Serikali, mishahara, OC na miradi ya maendeleo imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 37.51 kutoka bilioni 18 hadi bilioni 25.
- Serikali ya awamu ya sita imetoa kiasi cha zaidi ya bilioni tatu kwa ajili ya utoaji wa huduma za tiba na ushauri katika Hospitali ya Wilaya, Vituo vya afya na Zahanati za vijiji.
- Fedha kiasi cha zaidi ya bilioni moja kwa ajili ya shule za msingi.
- Fedha kiasi cha zaidi ya bilioni sita kwa ajili shule za sekondari.

# MHE. WAZIRI ASHANGAZWA NA KASI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO MASASI MJINI, ASEMA NI TAFSIRI SAHIHI YA KASI YA MHE. DKT. SAMIA

**WAZIRI** wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax (Mb) Oktoba 9, 2024 aliipongeza Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia wakati na muda uliopangwa huku ikiwa na viwango na ubora unaostahili.

"Nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa wote waliosimamia ujenzi wa madarasa haya, ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi wa Mji Ndg. Reuben Sixbert Jichabu, Mkuu wa Wilaya, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe, waheshimiwa madiwani wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi Mhe. Hashim Namtumba na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Patrick Sawala, wakati akitoa taarifa ya ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya sekondari Anna Abdallah ameeleza ujenzi ulianza mwezi wa nne na kukamilika mwezi wa sita. tunawapongeza sana kwa kukamilisha miradi ndani ya muda mfupi, hii haijawahi kutokea hata viwango na thamani ya pesa ni ya kuridhisha. **Hii inatafsiri pana kwamba Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan hana mchezo anataka kazi zake zifanyike na ziwe zina matokeo na matokeo yake ndo haya hapa,** namshukuru sana Mhe. Rais kwa kuona umuhimu wa afya na elimu."





*WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax (Mb) akizindua ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya sekondari Anna Abdallah*

Inaendelea Uk...05





WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax (Mb) akizindua ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya sekondari Anna Abdallah

# UZINDUZI WA ZAHANATI TATU KWA KISHINDO, ZAHANATI YA NAPUPA, ZAHANATI YA MATAWALE NA ZAHANATI YA MUMBAKA ,WANANCHI WANUFAIKA.






Inaendelea Uk...06

**ALIYEKUWA** Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe alizindua rasmi miradi mitatu ya Zahanati ikiwa ni Zahanati ya Napupa,Zahanati ya Matawale na Zahanati ya Machombe zinazolenga kusaidia na kupunguza umbali kwa wananchi kutafuta huduma za afya.

Mhe Mwambe alisema Ujenzi wa Zahanati hizo ni kiu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha huduma za afya zinawafikia Wananchi katika Kata zote 14 za Masasi Mji.

Aidha alimpongeza Mkurugenzi wa Mji Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu wa kukamilisha Miradi Vipolo yote katika mwaka wa Fedha 2023/2024.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi Mhe. Hashim Namtumba alisema kasi ya uzinduzi na ukamilis haji wa zahanati hizo, ni kuonesha namna ambavyo waheshimiwa madiwa ni wanavyosimamia Halmashauri na kuwasilisha suluhu ya changamoto za wananchi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu, alisisitiza kuwa watoa huduma za afya wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa wananchi na kuwahudumia kwa unyenyekevu kwani ndilo jukumu lao kama watoa huduma za Afya, hivyo basi wataweka boksi la maoni kwa wananchi ili waweze kutoa maoni yao juu ya utoaji huduma katika Zahanati hizo huku akisisitiza kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaendelea kufanyika kwa kasi na viwango vina vyostahili ili wananchi wa Halmas hauri ya Mji Masasi wafurahie maen deleo yanayofanywa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji Masasi Dkt. Salum Gembe, alisema kuwa Halmashauri ya Mji kwa sasa ina vituo 23 vya Afya vinavyofanya kazi kabla ya uzinduzi wa kituo cha Napupa, hivyo baada ya uzinduzi wa vituo hivyo idadi inaongeze ka na na kufikia vituo 24 ambapo vituo vya serikali 13 na vituo binafsi 11.

Uzinduzi wa Zahanati ya Napupa ulifanyika Agosti 2, 2024 uligharimu kiasi cha Tsh milioni 160, Uzinduzi wa Zahanati ya Matawale ulifanyika Novemba 24, 2023 uligharimu kiasi cha Tsh milioni 150 kutoka Serikali kuu na uzinduzi wa zahanati ya Machombe ulifanyika Novemba 18, 2023.



# DC MASASI MHE. KASSANDA AELEZA MAFANIKIO SEKTA YA MAJI NA BARABARA

**MKUU** wa Wilaya ya Masasi Mhe Rachel Kassanda akizungumza na wananchi April 7, 2025 katika Uwanja wa Sabasaba kuhusu mafanikio ya miaka minne ya nguvu ya Serikali ya awamu ya 6 alisema katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maji safi na salama Masasi jumla ya shilingi 11,955,101,755.05 zilipokelewa na wakala wa maji vijijini RUWASA na shilingi 1,038,332,009 zilipokelewa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachin gwea (MANAWASA) na 12,993,433,764.05 katika wilaya ya Masasi kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kupitia MANAWASA na RUWASA.

Alisema Miradi hiyo imetekelezwa ili kuhaki kisha wanachi wanapata maji ya kutosha na kupunguza umbali wa kufuata maji.

Aidha alisema kutokana na upatikanaji wa maji, serikali imewezesha Kumtua mama ndoo kichwani, Kuongezeka kwa uzalishaji kwakuwa muda mwingi waliokua wanatu mia wananchi kutafuta maji, kwasasa wanautumia kuzalisha mali na Kupungua kwa magonjwa yatokanayo na utumiaji wa maji yasiyofaa.

**Kuhusu Barabara** alisema shughuli za usafirishaji ni muhimu katika kukuza Uchu mi wa wilaya na Nchi kwa ujumla, Serikali yetu ya awamu ya 6 mpaka sasa imekwi shatuletea jumla ya shilingi 17,951,286,107.20 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa Baraba ra kupitia wakala wa Barabara vijijini-TARURA.

Miradi iliyotekelezwa ni ujenzi wa Barabara zenye urefu wa Km 14 kwa kiwango cha lami, Barabara zenye urefu wa Km 214.04 kwa kiwango cha changarawe na Barabara zenye urefu wa Km 1400.09 kwa kiwango cha udongo. Uwepo wa Barabara umechochea kukua kwa Uchumi .








# UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KISASA HOSPITALI YA MKOMAINDO. MILIONI 900 ZATOLEWA.

**UKARABATI** wa Hospitali ya Mkomaindo umeleta mabadiliko chanya kwenye sekta ya Afya Halmashauri ya Mji Masasi, Hospitali hii ipo katika Kata ya Mkomaindo na ilipokea fedha kutoka Serikali Kuu ambapo kiasi kilichotumika ni shilingi **milioni mia tisa (900,000, 000.00).**



*Muonekano wa Juu wa Majengo mapya hospitali ya Mkomaindo*

Hospitali ya Mkomaindo ilianzishwa mwaka 1951, na mwaka 1964 ilianza kuendeshwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanywa kuwa hospitali ya wilaya ya Masasi.

Hospitali ina vitengo vya huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD), wagonjwa wa ndani (IPD), huduma za maabara, meno, uchunguzi kwa mionzi, kifua kikuu, huduma za dharura, kliniki za baba, mama na mtoto (RCH) na huduma mbalimbali.




Fedha hizo zimejenga,Mradi wa kisasa wa Jengo la Mama na Mtoto, Umaliziaji wa OPD na Maabara, ukarabati wa jengo la kufulia, ukarabati wa mfumo wa majisafi na majitaka, ujenzi wa stoo ya dawa ya kisasa na ujenzi wa kichomea taka.





**Asante za wananchi** kwa Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za miradi yote ya Masasi, aliye kuwa Mbunge wa Jimbo la Masasi Mji ni Mhe.Geoffrey Mwambe kwa kuhaki kisha fedha za miradi zinakuja kwa wananchi Masasi na Baraza la Madi wani kwa usimamizi wa miradi yote ya maendeleo Halmashauri ya Mji Masasi.



# WAJUMBE WA KAMATI YA BUNGE WAPONGEZA UBORA WA KITUO CHA AFYA MTANDI.

**WAJUMBE** wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wamepongeza ubora wa miundombinu na vifaa tiba vya kutolea huduma za afya katika kituo cha afya Mtandi, Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara.

Aidha wamempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe kwa kupambana kwa kuhakikisha miradi mbalimbali ikiwemo kituo hicho inawafikia wananchi wote wa Masasi.




Inaendelea Uk...10

Pongezi hizo zimetolewa Novemba 13, 2023 mara baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Dennis Londo kutembelea na kukagua miundombinu katika kituo cha afya Mtandi.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Mbunge Mwita Waitara amesema vifaa tiba katika kituo hicho vina ubora mkubwa na vya kisasa

***"Mhe Mwenyekiti, Hapa wana mitambo ya kisasa kabisa, hapa, tumepita Dental service inayotolewa hapa, kwangu kule sijaiona, hivyo nimepiga picha nikawaoneshe wenzangu kwamba kule Masasi, Mtwara Kuchelee..sasa hii kazi ya Mama Samia lazima tuiseme, wananchi wajue kwamba hapa kuna kituo cha kisasa chenye vifaa vya kisasa" Mjumbe wa Kamati, Mbunge Mwita Waitara.***

Naye, Mjumbe wa kamati hiyo, Profesa Palamagamba Kabudi amesema kituo hicho kinafaa kuwa hospitali .

***“Nami niungane na wenzangu wote kuipongeza kabisa Halmashauri ya Mji Masasi na Wilaya kwa kujenga kituo cha afya cha viwango vya hali ya juu, kwasisi wahenga hiki sio kituo cha afya, hii ni hospitali, kwakweli viwango Vyake ni vya hospitali, kituo cha afya hiki baada ya miaka 10 au 15 kitakuwa hospitali. rai yangu tujitahidi tujenge uzio" Mjumbe wa Kamati, Profesa Kabudi.***

Aidha kwa niaba ya Mwenyekiti, Mjumbe wa kamati hiyo, Mbunge Amandus Chinguile ametoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais na Mbunge wa Jimbo hilo.

***"Nilete salamu za Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, Mhe. Geoffrey Mwambe, anafanya kazi nzuri sana, jamani hivi vitu havijileti huku kimiujiza, wako watu wanasema kwa niaba yenu, na huyo mtu ni mbunge wenu, anafanya kazi nzuri sana.***



*Kituo cha Afya Mtandi*

# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO UMEFANYIKA KWA KASI NA KIWANGO CHA JUU.

**BARAZA** la Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi likiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Hashim Namtumba limemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyowezesha ukuaji na ustawi wa wananchi wa Mji wa Masasi.

Baraza lilisema hayo Juni 20, 2025 wakati **"Baraza likivunjwa rasmi"** mara baada ya kutumikia wananchi katika kata zote 14 za Halmashauri ya Mji Masasi katika kipindi cha miaka mitano.



*Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya sekondari Temeke*



*Ujenzi wa maabara shule ya sekondari Temeke*



*Ujenzi wa Bweni shule ya msingi kwa elimu Jumuishi Masasi.*



*Ujenzi wa madarasa shule ya Namatunu*

Inaendelea Uk...12

***"Katika kipindi chetu tumetekeleza miradi mingi sana ya maendeleo, kila kata imefanikiwa kupata miradi mingi, kiupekee tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hakika wananchi wa Kata zote 14 wamenufaika na utekelezaji wa kishindo wa Miradi ya Maendeleo, kuanzia elimu, afya, maji, barabara, umeme , Tasaf kama tulivyoona kaimu mkurugenzi akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi kwa miaka yote hata mapato ya ndani yamepanda kutoka bilioni 1.8 hadi bilioni 4 ni hatua kubwa sana"***

Alisema hayo aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe. Hashim Namtumba akizungumza kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mabadiliko ya kihistoria yaliyofanyika .

Mkuu wa Wilaya Mhe. Rachel Kassanda aliwashukuru waheshimiwa madiwani kwa ushirikiano wao katika kipindi cha miaka mitano ya kuhakikisha wanasimamia ipasavyo utekelezaji wa miradi ya maendeleo na fedha zilizotolewa na Rais Dkt.Samia.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe alisema Masasi mpya imewezekana kutokana na ushirikiano bora uliopatikana kutoka kwa wananchi wa Masasi Mjini, waheshimiwa madiwani na watumishi wakiongozwa na Mkurugenzi wa Mji Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu kwa uimara wa uongozi wake.

Alisema miradi yote ililenga kuhakikisha wananchi wa Masasi wanafurahia mazingira na maisha.

Nao waliokuwa Madiwani , walitoa shukurani zao kwa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi na kwa kupata fedha za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata zao.



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri



Waheshimiwa Madiwani wakiwa katika Baraza

# NUKUU



Ndg. Reuben Sixbert Jichabu
Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Masasi

"Kama waheshimiwa madiwani mnavyokumbuka kwenye bajeti hii tunayoteke leza (2023/2024) tulitenga fedha kwaajili ya kumalizia miradi mbalimbali ikiwemo kumalizia shule ya sekondari Temeke, tayari fedha yake tumeshaikusanya,ipo tayari. inapofikia mwisho wa mwezi wa sita miradi yote itakuwa imekamilika. Lengo ni kuhaki kisha miradi iliyotengwa kwenye bajeti tunaitekeleza na kuikamilisha yote."



## RC MTWARA AKABIDHI MADAWATI 1500, ASEMA NI REKODI YA KIHISTORIA

**MNAMO** Januari 31, 2024, Rc Mtwara alizindua rasmi Madawati 1500 yenye thamani ya Tsh 112,500 ,000/= kwa ajili ya shule za msingi na awali Halmashauri ya Mji Masasi.

Rc aliambatana na wakuu wa wilaya zote za Mtwara na wakurugenzi wa Halmashauri zote mahususi kwaajili ya kuiga jambo hilo kubwa na kwenda kutekeleza kwenye maeneo yao.

Mkurugenzi wa Mji Masasi Ndg. Reuben Jichabu alisema mahitaji ya madawati kwa shule za msingi na awali yalikuwa ni 8443 na upungufu ulikuwa ni madawati 1891 hivyo upatikanaji wa madawati hayo ulimaliza kabisa changamoto ya madawati shuleni.

Wakikabidhiwa madawati hayo, walimu mbalimbali walisema madawati hayo yameleta suluhu kwa wanafunzi katika shule zao na hivyo kusaidia katika ufaulu.

**ELIMU KWA MLIPAKODI**

# LIPA USHURU

## NA LESENI

## KWA MAENDELEO YA

## HALMASHAURI YA MJI MASASI



# “MJI WETU, FAHARI YETU”

*Elimu kwa mlipakodi*

**Wasiliana nasi.**
Mkurugenzi wa Mji Masasi
Anuani ya Posta: P.o.box 447, Masasi
Simu ya Mezani: +255232510685
Barua pepe: info@masasitc.go.tz
Tovuti: www.masasitc.go.tz
Fb, Insta, Twitter (X), Youtube: halmashauri mji masasi

# BARAZA LA WAZEE MASASI LAPONGEZA UBORA WA HUDUMA ZA AFYA MASASI MJI




**BARAZA** la Wazee Masasi limeshangazwa na ubora wa vifaa tiba na miundombinu inayopatikana katika vituo vya kutolea huduma za Afya mara baada ya kutembelea Hospitali ya Mkomaindo, Kituo cha Afya Mtandi na Kituo cha Afya Mbonde huku wakimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa mabadiliko hayo ya kihistoria katika vituo vya kutolea huduma za Afya Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara.

Walisema hayo Julai 15, 2024 katika ziara ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe, Geoffrey Mwambe akiambatana na aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi,Mhe. Hashim Namtumba, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya Mhe. Ally Salvatory, Mganga Mkuu Dkt. Salum Gembe na wataalamu mbalimbali katika ziara hiyo mahususi kwa ajili ya Baraza la Wazee Masasi kutembelea vituo vya kutolea huduma za Afya.

Wakizungumza Katika ziara hiyo, wamesema mabadiliko waliyoyashuhudia ni ya kistoria na kuwaomba wananchi wafike katika vituo vya kutolea huduma za Afya kujionea wenyewe maboresho hayo makubwa ambayo hajayawahi kutokea kwa miaka mingi.

***“Wito wangu wananchi wengine waje Hospitali, ebu waje hospitali waone hospitali ilivyo bora, ilivyokuwa na mambo ya kisasa na ya kuridhisha na sisi Masasi tusiite masasi, napenda tuiite (New Masasi) kwa maana ya Masasi mpya, niwaombe wananchi wasiishie kusikia tu, waje wajionee wenyewe), Wamesema.***

Akizungumza katika ziara hiyo, Mhe Mwambe alisema mageuzi mbalimbali yamefanyika kuanzia majengo na vifaa tiba ili wananchi wa Masasi waweze kunufaika na huduma hizo.

“Kituo cha afya Mtandi na Kituo cha Afya Mbonde tumevijenga kwa ajili ya kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Mkomaindo na ili tubadili fikra ni muhimu Madaktari kutoa huduma kwa wakati, tuimarishe upande wa kujifungua,tuimarishe Upatikanaji wa dawa hospitali sambamba na huduma za mionzi”. Amesema

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi, Mhe. Hashim Namtumba alisema kazi kubwa imefanyika katika maboresho hayo kilichobaki ni kubadili fikra na mitazamo kwa wananchi ambao bado wanamitazamo hasi ya huduma za miaka ya zamani.

# DONDOO MUHIMU ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

- **UJENZI** wa shule mpya ya Sekondari Kata ya Jida, Mradi unapatikana kata ya Jida fedha iliyotolewa ni **shilingi 560,552,827.00.** Mradi huu umekamilika na unatumika.



- **UJENZI** wa shule mpya ya sekondari Matawale, kata ya Matawale, Fedha iliyoto lewa ni **shilingi 560,552,827.00.** Mradi huu umekamilika na unatumika.







Inaendelea Uk...17

- **UJENZI** wa shule mpya ya Sekondari Temeke, Mradi unapatikana kata ya Temeke, fedha iliyotolewa ni **zaidi ya milioni 839** sambamba na ujenzi wa mabweni. Mradi huu umekamilika na unatumika.





Inaendelea Uk..18

▶ **SERIKALI** ya awamu ya sita imetoa fedha kiasi cha Shilingi **Bilioni sita,** milioni sabini na moja,arobaini na tisa elfu mia nne kumi na tatu na senti sabini.6,071,049, 413.70 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu sekondari. Mafanikio yaliyop atikana katika sekta hii ni pamoja na:-

- Kujenga **matundu ya vyoo 93**, **vyumba 70 vya madarasa** pamoja na kutengeneza **viti na meza 3,360,** maabara **6** kujenga Nyumba za walimu 3 za mbili kwa moja na kujenga **mabweni 10 mapya** na **ukarabati wa mabweni mengine 8** katika shule za Sekondari 3. Pia umefanyika umaliziaji wa chumba cha TEHAMA 1, Maktaba 1 na maabara 3. Utekelezaji huu ume fanyika kwa fedha za UVICO,Kapu la Mama,SEQUIP na Mapato ya ndani.

- Ujenzi na usajili wa **shule mpya 3 za kata** (Sekondari Temeke, Sekondari Jida na sekondari Matawale na ujenzi wa **shule moja ya amali Marika** unaende lea.Utekelezaji huu umefanya ongezeko la shule za sekondari kutoka 9 hadi 12 na tunatarajia kuwa na shule 13 hadi kufikia Julai 2025.

- Nyumba za walimu zimeongezeka kutoka **nyumba 43 hadi 46** ambapo nyumba 3 za Mbili kwa moja (2 in 1 ) zimejengwa katika shule za Temeke Masasi,Jida na Marika.

- Idadi ya wanafunzi walioandikishwa kidato cha tano imeongezeka kutoka wanafunzi **275 mwaka 2021 hadi 730 mwaka 2025** na kwa kidato cha kwanza uandikishaji umeongezeka kutoka **wanafunzi 1,631** mwaka 2021 **hadi 2,017** mwaka 2025.

## DONDOO MUHIMU ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ELIMU MSINGI

▶ **SERIKALI** ya awamu ya sita imetoa fedha kiasi cha **Shilingi 1,066,430,592** kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na:-

- Kujenga na kukamilisha **matundu ya vyoo 142, vyumba 105 vya madarasa** pamoja na upatikanaji wa **madawati 3,075 katika shule 42** za Msingi.Uteke lezaji huu umefanyika kwa fedha kutoka Serikali Kuu, Mradi wa Boost, Lipa kwa Matokeo (EP4R),GPE LANES II, TRA na Mapato ya ndani na nguvu za wananchi.

Inaendelea Uk...19

- **UJENZI** wa shule mpya ya Msingi Darajani, Mradi unapatikana kata ya Mkomaindo fedha iliyotolewa ni zaidi ya **milioni 331**. Mradi huu umekamilika na unatumika.



- **UJENZI** na usajili wa **shule mpya 3** na kufanya ongezeko la shule za Msingi kutoka 39 hadi 42.Nyumba za walimu na ofisi za walimu zimeongezeka kutoka nyumba **37 hadi 42** na ofisi kutoka **58 hadi 72.**

- **IDADI** ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa kuhitimu darasa la saba imeongezeka kutoka na **wanafunzi 1,923 hadi 2,361** kwa mwaka 2024.

## DONDOO ZA MAFANIKIO SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

- **KUONGEZEKA** kwa idadi ya biashara zilizorasimishwa kwa utoaji wa leseni za biashara kutoka **biashara/leseni 860 hadi kufikia 1980** Juni 2025.

- Kuongezeka kwa idadi ya Viwanda.Viwanda **vidogo sana 89 hadi 117**,viwanda **vidogo 9 hadi 20** na viwanda vya **kati 0 hadi 3** na viwanda **vikubwa 2 hadi 3** mwaka 2025.

- Uwepo wa viwanda hivi vimepelekea ajira **kuongezeka kutoka 250 hadi 478** mwaka 2025

Inaendelea Uk...20

- Uwekezaji mbalimbali ikiwemo ujenzi wa majengo **makubwa 2** ya biashara ambayo yana uwezo wa kuhudumia wafanyabiashara **wasiopungua 150** yaliyopo kata ya Mkuti na kata ya Jida na kuongezeka kwa nyumba za kisasa za kuhudumia wageni na kufanya **idadi ya nyumba kutoka 64 hadi 110.**

## DONDOO ZA MAFANIKIO SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

- **IDADI** ya kuku waliochanjwa dhidi ya ugonjwa wa kideri imeongezeka kutoka kuku **112500 kwa mwaka 2021 hadi 385500** kwa mwaka 2025.

- Kuongezeka kwa huduma bora za ugani baada ya maafisa ugani kupata vyombo vya usafiri (pikipiki) 2021 hadi kufikia **pikipiki 22 kwa mwaka 2025**.

- Kwa msimu wa 23/24 Serikali imefanikiwa kuwasambazia wakulima pembejeo za zao la korosho salfa ya **unga Kg 788,750** na viuatilifu vya **maji Lita 27,365.** Aidha kwa msimu wa 2024/2025 Sulfa ya unga ni **Kg 837,350** na viuatilifu vya maji ni Lita 28,234 na viuatilifu hivyo vyote vinatolewa kwa **ruzuku ya asilimia 100(100%).**

- Idadi ya mifugo iliyopata chanjo dhidi ya ugonjwa Kideli na kichaa cha mbwa imeongezeka kutoka **Kuku 1,258 hadi 32,185, Mbwa 1,582 hadi 4,840 na Paka 219 hadi 796.**

## DONDOO ZA MAFANIKIO SEKTA YA FEDHA

- **KATIKA** kipindi cha Serikali ya awamu ya sita, Halmashauri imeweza kupandisha bajeti ya makisio ya **mapato ya ndani** kutoka Shilingi **2,370,676,543** mwaka 2021 hadi **Shilingi 3,397,213,000** mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la **asilimia 43.30** na makusanyo yameongezeka kutoka **1,856,478,321.94** mwaka 2021 hadi **bilioni 4,299,107,143** mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la **asilimia 131.57** ambayo itaendelea kuchangia katika uendeshaji wa Halmashauri na miradi ya Maendeleo kwa wananchi.

- Ruzuku kutoka **Serikali kuu** kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo imeendelea kongezeka kutoka **shilingi 18,738,500,358** kwa mwaka 2021 hadi kufikia **shilingi 25,766,864,953** mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la **asilimia 37.51** ambayo kwa kiasi kikubwa imechangia katika uende shaji wa shughuli za Halmashauri na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi.

# DONDOO ZA MAFANIKIO SEKTA YA USAFI WA MAZINGIRA NA UDHIBITI TAKA

**KATIKA** kipindi cha Serikali ya awamu ya sita, shughuli za usafi wa mazingira zimezidi kuimarishwa na kuboreshwa ambapo Chini ya Mkurugenzi wa Halmash auri ya Mji Masasi **Ndg. Reuben Sixbert Jichabu** Halmashauri kupitia mapato ya ndani imefanikiwa kununua **lori mpya** la Taka lililogharimu kiasi **cha milioni 141** ili kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo ya mji na masoko.



## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO 2024/2025

**SERIKALI** ya awamu ya sita inayoongozwa na **Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuvunja rekodi za kihistoria katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo** ambapo kipekee **Halmashauri ya Mji Masasi** mwishoni mwa mwaka wa fedha **2023/2024** ilipokea f**edha kiasi cha Tsh. 3, 030, 296, 586.74** (**zaidi ya bilioni 3**) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo hadi Juni 30, 2025 kwa asilimia nyingi miradi hiyo imekamilika na inatumika na wananchi wa Halmashauri ya Mji Masasi.

**Dondoo jumla ya miradi 15** yenye thamani ya **zaidi ya shilingi bilioni 3.5** imetekelezwa:, kama inavyoonekana kwenye kurasa inayofuata:-

Inaendelea Uk...22

Inatoka Uk...21

- Ujenzi wa shule ya sekondari ya Amali Marika, Fedha iliyotolewa ni **shilingi bilioni 1.6**



- Ujenzi wa shule **mpya ya sekondari Matawale,** Fedha iliyotolewa ni shilingi **milioni 560,552,827.00, mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa madarasa 4, matundu 10 ya vyoo na mabweni 2 shule ya Sekondari **Temeke Masasi,** Fedha iliyotolewa ni **shilingi 369,000,000, mradi huu umekamilika na unatumika.**
- **Ukarabati wa mabweni 2** shule ya **Sekondari Mtapika**, Fedha iliyotolewa ni shilingi **158,417,625.89, mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa **Machinjio mpya** unaofanyika Kata ya Mtandi wenye thamani ya zaidi ya **Tsh milioni 244** kupitia fedha za mapato ya ndani.
- Ujenzi wa **standi ya Maegesho ya vyombo vya moto** kata ya Mwengemtapika uliogharimu zaidi ya **Tsh milioni 100 fedha za mapato ya ndani. Mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa **nyumba za walimu 2 kwa 1** shule ya **Msingi Matawale,** Fedha iliyotolewa ni **shilingi 95,000,000, mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa nyumba za **walimu 2 kwa 1 Jida Sekondari,** Fedha iliyotolewa ni **shilingi 95,000,000, mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa **nyumba za walimu 2 kwa 1 kituo cha Afya Mtandi,** Fedha iliyotolewa ni **shilingi 95,000,000 fedha za mapato ya ndani, mradi huu umekamilika na unatumika.**

Inaendelea Uk..23

Inatoka Uk...22

- Ujenzi wa Vyumba 3 vya madarasa na matundu 6 ya vyoo shule ya msingi Mkuti B, Fedha iliyotolewa ni shilingi 83,200,000, **mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 6 ya vyoo shule ya Msingi Sabasaba, Fedha iliyotolewa ni shilingi 59,200,000, **mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 6 ya vyoo shule ya Msingi Namatunu, Fedha iliyotolewa ni shilingi 83,200,000, **mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ukarabati wa mabweni 2 shule ya Sekondari Sululu, Fedha iliyotolewa ni shilingi 86,726,133.8**, mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ujenzi wa madarasa 2 na matundu 2 ya vyoo Shule ya Msingi Nangose, Fedha iliyotolewa ni shilingi 52,200,000, **mradi huu umekamilika na unatumika.**
- Ukamilishaji wa chumba 1 cha Maabara shule ya Sekondari Sululu, Fedha iliyotolewa ni shilingi 30,000,000, **mradi huu umekamilika na unatumika.**

## UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

***Halmashauri ya Mji Masasi imeweza kutoa mikopo kiasi cha Tshs 1,246,483,003. kwa jumla ya vikundi 241 kati ya hivyo vikundi vya wanawake 157,vikundi vya vijana 71 na Vikundi vya watu wenye ulemavu 13.Aidha jumla ya wanachama 1524 wamenufaika na mikopo ya asilimia kumi (Wanawake 1028,Vijana 469 na Wenye ulemavu 27).***

## UTEKELEZAJI WA MRADI WA UFUNGAJI WA TAA ZA BARABARANI





**KATIKA** kipindi cha Serikali ya awamu ya sita, Halmashauri ya Mji Masasi kupitia kwa Mkurugenzi wa Mji Masasi Ndg. Reuben Jichabu,lililokuwa Baraza la Madiwani na aliyekuwa Mbunge Mhe. Geoffrey Mwambe, Halmashauri imefanikiwa kufunga taa za barabarani katika barabara mbalimbali ndani ya mji ili kuwezesha wafanyabias hara kufanya biashara muda wote na kuimarisha ulinzi na madhari ya Mji wa Masasi.

**Jumla ya Taa 190** zenye thamani ya **zaidi Tsh milioni 575,** zimefungwa katika barabara mbalimbali ndani ya Mji. Barabara hizo:-

***Masasi-Navai, Tanesco-Yatima, Yatima-Machinjioni, Sokoni -Machinjio, Posta-Mkapa, Ujenzi -jida, Barabara Mefu(Kibo), Uwanja wa Boma na Maegesho ya Vyombo vya Moto.***

## MICHEZO

# UKARABATI WA KISASA WA UWANJA WA BOMA UNAENDELEA



**HALMASHAURI** ya Mji Masasi kupitia Mfuko wa Jimbo imetoa fedha zaidi ya **milioni 54** kwaajili ya utekelezaji wa kisasa wa ukarabati wa Uwanja wa Boma uliopo Kata ya Nyasa ili uweze kusaidia wananchi wa Masasi kwenye michezo na kuongeza mapato ya Halmashauri.

Katika hatua za mwanzo tayari ukarabati wa vyoo na ukuta vimefanyika, kufanikiwa kutoa mwamba mgumu uliokuwa kwenye uwanja, kufukua na kutoa udongo usiofaa, upimaji wa vipimo vya uwanja umekamilika na hatua zinazofuata ikiwemo kuweka udongo mbolea, kuweka miundombinu ya kisasa ya maji na kupanda nyasi za kisasa.

Katika hatua nyingine tayari taa mbalimbali zimefungwa uwanjani hapo ili kuwezesha michezo na burudani kufanyika nyakati zote za usiku na mchana kwa ubora na ufanisi uliokusudiwa.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe alisema Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imejizatiti kuhakikisha inaboresha na kuimarisha mazingira bora ya michezo Halmashauri ya Mji Masasi.

## MATUKIO KATIKA PICHA




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia wananchi wa Masasi Sep. 13, 2023 katika Uwanja wa Boma, Halmashauri ya Mji Masasi




Maelfu ya wananchi wa Masasi waliojitokeza kumpokea na kumsikiliza Mhe.Dkt. Samia Sep.13, 2023 uwanja wa Boma Halmashauri ya Mji Masasi



Jengo la Utawala/ Ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Masasi, Wananchi hufika na kupata huduma mbalimbali.




Wodi ya wazazi kituo cha Afya Mtandi, Mama wajawazito wanajifungua sehemu salama na yenye vifaa vya kisasa.

## Asante na Karibu

**Mawasiliano**

**Mkurugenzi wa Mji Masasi**
**Anuani ya Posta: P.o.box 447, Masasi**
**Simu ya Mezani: +255232510685**
**Barua pepe: info@masasitc.go.tz**
**Tovuti: www.masasitc.go.tz**
**Fb, Insta, Twitter (X), Youtube: halmashauri mji masasi**

Jarida la Mtandaoni limeandaliwa na,
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Mji Masasi